

HALMASHAURI YA MJI HANDENI



SHULE YA SEKONDARI KONJE

Kumb Na.kss/A/Vol1/11

Jina la Mwanafunzi

MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021 SHULE YA SEKONDARI KONJE.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2021 katika shule hii nimatumaini yangu utaitumia nafasi hii vizuri. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021 hivyo ufike siku hiyo saa 1;00 asubuhi bila kukosa.

1.0. MZAZI

Muandae mwanao vizuri ili aweze kusoma na kupata mafanikio. Kama utampangishia mwanao, kwa wale wanaotoka mbali ni vema uhakikishe usalama wa sehemu hiyo uweke uangalizi wa karibu vinginevyo utaingia hasara. Usifanye kosa la kumuamini mwanao kwa asilimia mia. Pia mnunue mwanao begi la shule, kaunta buku 10, mkebe wa hisabati, rula ma kalamu za kutosha.

2.0. SARE ZA SHULE

Sare ya shule hii ni shati jeupe lenye mikono mifupi, soksi nyeupe na viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba kwa wavulana na wasichana pamoja na flana za shule (T-shirt) ambazo zitapatikana shule kwa gharama ya elfu kumi (10,000) ambazo zitavaliwa mara mbili kwa kila wiki, jumatano na ijumaa. Siku ambazo wanafunzi hawatoruhusiwa kuvaa shati za shule.

2.1. Wavulana washone suruali za kitambaa rangi ya damu ya mzee mshono wa kawaida wenye marinda suruali iwe pana na ndefu.

2.2. Wasichana washone sketi ndefu zenye linda 8 hadi 10

Kila sare ni pea mbili wanaotaka kuvaa hijabu wanapaswa kushona na kitambaa cheupe kisichokuwa na mapambo, hijabu iwe ndefu inayofika kwenye vidole. Vazi la suruali kwa Wasichana HALIRUHUSIWI shuleni.

2.3. Kila mwanafunzi lazima anunuliwe raba za michezo, bukta na flana.

3.0. Kila mwanafunzi aje na fagio la chelewa pamoja na ndoo ndogo kwa ajili ya usafi wa kila siku.

3.1. Siku ya kuripoti mwanafunzi aje na kwanja au fyekeo na jembe kwa ajili ya usafi wa maeneo ya nje pamoja na kulimia.

3.2. Mwanafunzi lazima apimwe afya yake na Mganga (HOSPITALINI) anayetambulika na Mhuri ugongwe panapohusika ,fomu kwa shughuli hiyo imeambatanishwa.

4.0. SHERIA ZA SHULE

Baadhi ya sheria muhimu za shule zimeambatanishwa na mwanao anaagizwa kuzisoma na kuzizingatia ili asome bila shida.

5.0. TAARIFA YA MAENDELEO

Kila inapofungwa shule hakikisha mwanao anakupatia ripoti yake ya maendeleo ya shule ili wewe upate nafasi ya kumshauri kimaadili na kitaaluma.

SHERIA ZA SHULE

Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

(a) Uasherati na ushoga

(b) Ubakaji

(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyo kama vile uvutaji bangi,cocain,mirungi,kubeli na kudhalika.

(d) Wizi

(e) Kupigana au kupiga

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule (UMMA)

(g) Kudharau Bendera ya Taifa

(h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba/Kutia mimba

(i) Kutoa mimba

(j) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu

(k) Kukataa adhabu kwa makusudi

(l) Kuwa na simu ya mkononi

(m) Kutohudhuria vipindi darasani bila taarifa

(n) Kutofanya kazi za darasani na nje ya darasa

MARY P. KILEO

MKUU WA SHULE

NB: Atakayeshona suruali ya kubana au sketi au hijabu au nusu kanzu sheria kali zitachukuliwa dhidi yake. Siku ya kufungua shule mwanafunzi lazima aletwe na mzazi wake iwapo ataripoti shuleni bila ya kuletwa na mzazi hatapokelewa.

KONJE SECONDARY SCHOOL
MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by medical officer in respect of Form I/V Entrants

Pupils full Name.....

Age.....

Blood cont (Red and white).....

Stool :.....

Urinalysis.....

Syphilis Test.....

T.B. Test :.....

Ears.....

Chest.....

Spleen:

Abdomen.....

ADDITION INFORMATION:

eg. Physical defects or impairments, infection, chronic or family diseases etc.

.....
.....
.....

Test pregnant for girls

students.....

.....
.....

I certify the above is fit/unfit for admission into a secondary school

Designation.....

Station.....

Date.....

Official stamp: